

MKOA WA TANGA:



S.L.P 89,  
PANGANI.

08/01/2017.

## TANGAZO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imepokea fedha shilingi **MILIONI MIA NNE (TZS 400,000,000/=) KUTOKA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (TAMISEMI).**

Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya Mwera. Ujenzi na ukarabati huo utahusisha, **Ujenzi wa chumba cha Upasuaji, Wodi ya Akina mama Wajawazito (Maternity ward), Wodi ya Watoto, Chumba cha kuhifadhi maiti na Maabara.** Miundombinu mingine ni pamoja na jengo la **kufulia nguo (Dobi), Kichomea taka, nyumba ya mtumishi, Mfumo wa uvunaji maji na Shimo la kutupia Kondo la nyuma.**

Pamoja na ukarabati wa miundombinu chakavu mingine ya Kituo cha Afya Mwera.

Aidha nawajulisha wananchi kuwa mradi huu unatekelezwa kwa kutumia utaratibu wa kununua vifaa (Force Account) na kuwatumia mafundi wajenzi (Local fundi). Muda wa utekelezaji wa mradi ni siku 90 (miezi mitatu).

Wananchi pamoja na wadau wote wa maendeleo mnatakiwa kutoa ushirikiano ili kuhakikisha lengo la serikali katika utekelezaji wa mradi huu linatimia.

Wananchi wote wa Pangani mnatakiwa kushiriki kwa hali na mali ili kufanikisha ujenzi huu kwa faida ya wakazi wa Mwera, Pangani na wananchi wote kwa ujumla.

Ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu.

  
Sabas D. Chambasi

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
PANGANI

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
PANGANI

Nakala:

*Mbao zote za matangazo ndani ya Wilaya ya Pangani.*